



**Universal**

**UNIVERSAL LEAF TOBACCO COMPANY, INC.**

**Ni sera ya Universal kwamba Universal na washirika wake, na maafisa wao husika, wakurugenzi, wafanyikazi na maajenti hawatauzi tobako makusudi kwa shirika lolote au mtu yoyote binafsi anayehusika na utengenezaji, usambazaji au uuzaji wa bidhaa bandia za tobako. Mtu yoyote anayekiuka sera hii, au anayeidhinisha, anayeruhusu au anasamehe ukiukaji wa mtu yoyote wa sera hii makusudi, atachukuliwa hatua kali ya nidhamu.**

Kumekuwa na tahadhari kubwa kutoka kwa umma na sekta kuhusu utengenezaji, usambazaji, na uuzaji haramu wa bidhaa bandia za matumizi za tobako, hasa sigara. "Bidhaa bandia za tobako" ni bidhaa zinazouzwa zikiwa na jina la mtu mwingine au nembo ya biashara au muundo wa kampuni ingine ili kudanganya wateja kuhusu ubora au asili ya bidhaa hiyo.

Sheria mbalimbali za madai na jinai zinaharamisha kusaidia au kushiriki kwa makusudi katika utengenezaji au uuzaji wa bidhaa bandia. Kama mchuuzi wa majani, Universal haiuzi bidhaa za matumizi za tobako, tunaumizwa na bidhaa hizo bandia kwa sababu biashara yetu inalenga huduma kwa makampuni ambayo chapa zao imara za bidhaa za tobako ndio zinazolengwa kwanza na biashara ya bidhaa bandia.

Kwa kukubaliana na sera yetu ya kupambana na bidhaa bandia, Universal imeanzisha mchakato ulioundwa kuthibitisha kwamba wateja wetu hawajihusishi na biashara ya bidhaa bandia na kwamba maajenti wetu hawasaidii biashara ya bidhaa bandia makusudi. Universal pia itafanya ukaguzi wa uzingatiaji wa mara kwa mara, ambao utajumuisha kukagua mchakato wa uthibitishaji wa mteja, ajenti, na itafuatatilia maendeleo yoyote maalumu katika upande wa bidhaa bandia ambayo yatafichuliwa kwetu kupitia vyombo vya habari, waasiliani wa serikali, na kupitia wafanyikazi na wateja wetu. Wateja na maajenti wetu wote wa sasa na wa siku zijazo watajulishwa masharti ya sera yetu na watahamasishwa kutujulisha kuhusu maendeleo mapya katika upande wa bidhaa bandia.

Universal imejitolea kuwa na sera madhubuti ya kupambana na bidhaa bandia. Kila mtu katika familia ya Universal lazima afikirie jinsi sera hii inaweza kutumika katika muamala, shughuli, au utendaji wowote maalumu ambao wanajihusisha nao. Maswali au masuala yoyote yanayohusika na sera hii yanafaa yaelekezwe kwa Idara ya Kisheria ya Universal, na Idara ya Kisheria inafaa iarifiwe kuhusu ukiukaji wowote wa sera hii.